Filemoni

1 Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu, pamoja na
Timotheo ndugu yetu:
Kwa Filemoni rafiki yetu mpendwa na mten-
dakazi mwenzetu,
2 kwa dada yetu mpendwa Afia, kwa Arkipo
askari mwenzetu na kwa kanisa lile likutanalo
nyumbani mwako:
3 Neema iwe nanyi na amani itokayo kwa
Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

Shukrani Na Maombi

4 Siku zote ninamshukuru Mungu
ninapokukumbuka katika maombi yangu,
5 kwa sababu ninasikia juu ya imani yako
katika Bwana Yesu na upendo wako kwa
watakatifu wote.
6 Naomba utiwe nguvu katika kuishuhudia
imani yako, ili upate kuwa na ufahamu mkamil-
ifu juu ya kila kitu chema tulicho nacho ndani
ya Kristo.
7 Upendo wako umenifurahisha mno na kuni-
tia moyo, kwa sababu wewe ndugu, umeiburud-
isha mioyo ya watakatifu.

Maombi Ya Paulo Ya Kumtetea Onesimo

8 Hata hivyo, ingawa katika Kristo ningeweza
kuwa na ujasiri na kukuagiza yale yakupasayo
kutenda,
9 lakini ninakuomba kwa upendo, mimi Paulo,
mzee na pia sasa nikiwa mfungwa wa Kristo
Yesu,

10 nakuomba kwa ajili ya mwanangu
Onesimo,* aliyefanyika mwanangu nilipokuwa
kwenye minyororo.
11 Mwanzoni alikuwa hakufai, lakini sasa
anakufaa sana wewe na mimi pia.

12 Namtuma kwako, yeye aliye moyo wangu
hasa.
13 Ningependa nikae naye ili ashike nafasi yako
ya kunisaidia wakati huu nikiwa kifungoni kwa
ajili ya Injili.
14 Lakini sikutaka kufanya lolote bila idhini
yako, ili wema wowote uufanyao usiwe wa
lazima, bali wa hiari.
15 Huenda sababu ya yeye kutengwa nawe kwa
kitambo kidogo ni ili uwe naye daima.
16 Si kama mtumwa, bali bora kuliko mtumwa,
kama ndugu mpendwa. Yeye ni mpendwa
sana kwangu na hata kwako zaidi, yeye kama
mwanadamu na kama ndugu katika Bwana.

17 Hivyo kama unanihesabu mimi kuwa
mshirika wako, mkaribishe kama vile un-
genikaribisha mimi mwenyewe.
18 Kama amekukosea lolote au kama unamdai
chochote, nidai mimi.
19 Ni mimi Paulo, ninayeandika waraka huu
kwa mkono wangu mwenyewe. Nitakulipa.
Sitaji kwamba nakudai hata nafsi yako.
20 Ndugu yangu, natamani nipate faida kwako
katika Bwana, uuburudishe moyo wangu katika
Kristo.

---

* **1:10** Onesimo maana yake ni Wa manufaa.

21 Nikiwa na hakika ya utii wako, nakuandikia,
nikijua kwamba utafanya hata zaidi ya yale
ninayokuomba.
22 Jambo moja zaidi: Niandalie chumba cha
wageni, kwa kuwa nataraji kurudishwa kwenu
kama jibu la maombi yenu.

Salamu Za Mwisho Na Dua Ya Kuwatakia Heri

23 Epafra, aliye mfungwa mwenzangu katika
Kristo Yesu, anakusalimu.
24 Vivyo hivyo Marko, Aristarko, Dema na
Luka, watendakazi wenzangu wanakusalimu.
25 Neema ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja na
roho zenu. Amen.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™ (Bible)

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.
You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.
Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 1 Oct 2024 from source files dated 31 Aug 2023
9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462